

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MADINI  
CHUO CHA MADINI DODOMA  
S. L. P 1696, Dodoma

Simu: +255 26 2300472, Fax: +255262963003  
Barua pepe: [info@mri.ac.tz](mailto:info@mri.ac.tz)/[principal@mri.ac.tz](mailto:principal@mri.ac.tz)/[registrar@mri.ac.tz](mailto:registrar@mri.ac.tz)  
Tovuti: [www.mri.ac.tz](http://www.mri.ac.tz)



**(Kimepewa Ithibati kamili na NACTE)**

## **NAFASI ZA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA NGAZI YA ASTASHAHADA/STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020**

Chuo cha Madini ni Chuo cha Serikali kipo chini ya Wizara ya Madini, kina uzoefu wa zaidi ya miaka thelathini (30) katika kufundisha wataalamu wa ngazi ya kati katika sekta ya madini. Mnamo mwaka 2012, Chuo cha Madini kilianza pia kutoa mafunzo katika sekta za Mafuta, Gesi na Mazingira; na mwaka 2018 Chuo kilianza kutoa mafunzo ya Upimaji Ardhi na Migodi. Chuo cha Madini kina ithibati kamili ya Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada hadi Stashahada (NTA level 4 - 6) katika mfumo wa umahili (CBET). Chuo cha Madini kinakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa kuomba nafasi za masomo kwa ngazi ya Astashahada/Stashahada kwa kozi zifuatazo:

- **Jiolojia na Ufafutaji Madini (Geology and Mineral Exploration)**
- **Uhandisi Migodi (Mining Engineering)**
- **Uhandisi Uchenjuaji Madini (Mineral Processing Engineering)**
- **Sayansi ya Mafuta na Gesi (Petroleum Geosciences)**
- **Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini (Environmental Engineering and Management in Mines)**
- **Upimaji Ardhi na Migodi (Land and Mine Surveying)**

### **SIFA ZA KUJIUNGA**

- Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne (Form IV) na awe amefaulu masomo ya Fizikia, Kemia, Hisabati na masomo mengine mawili (2) yasiyo ya dini kwa kiwango cha kuanzia D.
- Awe na cheti cha kidato cha nne (Form IV) na kufaulu masomo manne (4) ya sayansi (Kwa waombaji wa kozi ya Upimaji Ardhi na Migodi-*Land and Mine Surveying* tu)

### **NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

*Waombaji wote wenye sifa wanatakiwa kujaza fomu za maombi na kuzituma Chuoni moja kwa moja. Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Madini Kampasi ya Dodoma na Nzega, Ofisi za Wizara ya Madini, Ofisi za Madini zilizopo Mbeya, Tabora, Mwanza, Kahama, Dar es Salaam, Musoma, Songea, Arusha, Tanga, Tunduru, Dodoma, Morogoro, Handeni, Merelani, Mpanda, Bukoba, Mtwara, Shinyanga, Chunya, Moshi, Nachingwea, Geita, Bariadi, Singida na Kigoma, au katika tovuti ya chuo: [www.mri.ac.tz](http://www.mri.ac.tz)*

*Kwa maelezo/msaada zaidi wasiliana nasi kupitia: 0784 893 116 / 0764 910 385 / 0712650177 / 0753 858 028*

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 15/9/ 2019 saa 9:30 alasiri.**

Tarehe ya kuanza masomo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 ni 14/10/2019.

**NB:**

- Maombi yote yatumwe Chuoni ndani ya muda uliopangwa
- Fomu za maombi ziambatanishwe na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay-in Slip) yenye kiasi cha Tshs. 10,000/= na ilipwe kwenye akaunti ya Chuo (Akaunti Na. 01J1082316900, CRDB, CHUO CHA MADINI DODOMA).
- Wanawake wanahamasishwa zaidi kutuma maombi
- Chuo hakitoi ufadhili kwa wanafunzi watakaochaguliwa katika kozi zote

Fomu za maombi zitumwe kwa:

**Mkuu wa Chuo,  
Chuo cha Madini Dodoma,  
S. L. P 1696,  
Dodoma**